**WIZARA YA AFYA**

**HOTUBA YA MGENI RASMI: WAZIRI WA AFYA MHE. UMMY MWALIMU (MB)**

**KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MCHANGIA DAMU DUNIANI – MKOA WA SONGWE TAREHE 14 JUNI, 2022**

**Mhe. Mkuu wa Mkoa**

**Mhe. Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi - Mkoa wa Songwe**

**Mheshimiwa Mbunge wa (Jimbo)**

**Wakuu wa Wilaya (Wilaya)**

**Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya**

**Mhe. Naibu Katibu Mkuu – OR-TAMISEMI**

**Mwakilishi Mkazi Shirika la Afya Duniani**

**Katibu Mkuu – Tanzania Red Cross Society**

**Mwakilishi Mkazi Shirika la AMREF**

**Wakurugenzi Wizara ya Afya**

**Wakurugenzi Idara zote za OR-TAMISEMI**

**Mkurugenzi Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mbeya**

**Waganga Wakuu wa Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Songwe**

**Mganga Mfawawidhi Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe**

**Watumishi wote wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama**

**Watumishi wote wa sekta ya afya**

**Ndugu Waandishi wa Habari**

## Ndugu Wachangia damu - Wawakilishi wa Wachangia damu wa Mikoa yote ya Tanzania

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha wote kukusanyika hapa siku ya leo. Naamini na kumuomba aendelee kutulinda na kuifanya siku yetu ikaishe salama.

Nitumie pia fursa hii kuwashukuru wote mliojitolea muda wenu kujumuika na sisi leo katika tukio hili muhimu kwa afya na ustawi wa Wananchi wetu na Taifa letu kwa ujumla.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Tarehe 14 ya mwezi Juni ya kila mwaka, Tanzania huungana na nchi nyingine kuadhimisha Siku ya Wachangia Damu Duniani. Lengo la Siku hii ni kutambua na kuthamini wale wote wanaojitolea kuchangia damu kwa ajili ya kuokoa maisha ya wahitaji. Kila mwaka katika kuadhimisha siku ya wachangia damu duniani, Shirika la Afya Duniani hutoa kaulimbiu na malengo ya maadhimisho ambayo hutumika na nchi zote washirika, ambapo kwa mwaka 2022 kauli mbiu inasema **"KUCHANGIA DAMU NI KITENDO CHA MSHIKAMANO, TUUNGANE KUOKOA MAISHA"** (*"Donating blood is an act of solidarity. Join the effort and save lives").* Kauli mbiu hii inasisitiza na kuhamasiha jamii kuendelea kuchangia damu kwa hiari kwani kuchangia damu kunaleta upendo na mshikamano kwa sisi wenyewe, wale tunaowasaidia na jamii kwa ujumla.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama inaadhimisha sherehe hizi kwa kutambua na kuthamini mchango mkubwa wa wachangia damu nchini kwa utayari wao wa kujitolea kuchangia damu kwa wagonjwa wenye uhitaji. Pia Maadhimisho haya yanatumika kutambua mchango wa taasisi na vikundi mbalimbali ambavyo vimekuwa vikishirikiana na Wizara ya Afya katika kufanikisha upatikanaji wa damu salama nchini

ikiwemo kutoa elimu na kuhamasisha jamii ili kuona umuhimu wa kuchangia damu kwa hiari.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Naomba nichukue nafasi hii kuongea kuhusu hali ya upatikanaji damu nchini. Ili kuhakikisha kwamba kila mgonjwa anayehitaji tiba ya damu anapata damu salama, Shirika la Afya Duniani linapendekeza kukusanywa idadi ya chupa za damu ambazo ni sawa na asilimia 1 ya idadi ya wananchi waliopo kwenye nchi au eneo hilo kwa wakati huo. Kwa nchi ya Tanzania, ikikadiria kuwa tuna wananchi milioni 55, inatakiwa kukusanya chupa za damu 550,000 ambayo ni sawa na asilimia 100 ya mahitaji ya nchi ikilinganishwa na idadi ya wananchi waliopo. Takwimu za ukusanyaji damu, zimeonyesha kuwa na mafanikio ya kuongozeka kwa ukusanyaji damu mwaka hadi mwaka. Mwaka 2017/2018 jumla ya chupa za damu 257,557 ambayo ni sawa na 45% ya mahitaji zilikusanywa, kufanyiwa vipimo vya maabara, na kusambazwa. Idadi hii imeongezeka hadi kufikia chupa 312,714 sawa na 57% ya mahitaji kwa mwaka 2019/2020, na kufikia 331,279 ambayo ni sawa na 60% ya mahitaji ya nchi kwa mwaka 2020/2021.

Pamoja na ongezezo hilo, bado hatujafikia malengo ya kukusanya chupa 550,000 kwa kuwa ingawa chupa zilizokusanya mwaka 2022/2021 ni chupa 331,279 sawa na asilimia sitini (60%), bado kuna pungufu ya chupa 218,721 sawa na 40% ya mahitaji ya nchi. Kwa hiyo, ndugu wananchi, bado kuna kazi ya kufanya ya kuhakikisha tunaziba hilo pengo la asilimia 40 ili kukidhi mahitaji ya damu na kuhakikisha kuwa wale wote ambao wanahitaji kuongezewa damu wanapata huduma hio kwa wakati, na kwa viwango na kiasi kinachohitajika. Hivyo ushiriki wa taasisi na vikundi mbalimbali katika kutoa elimu na kuhamasisha jamii kuchangia damu ni muhimu sana ili kuweza kupunguza na hatimae kuondoa pengo lililobaki na kuondoa kabisa uhaba wa damu. Tunahitaji kuungana pamoja, kuendelea kuhamasisha jamii kujitolea kuchangia damu kwa hiari, na kufanya hivyo mara kwa mara.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Wengi wetu tunajua kuwa wachangiaji damu huokoa maisha kila siku kupitia zawadi yao ya uhai kupitia uchangiaji wa damu. Kila sekunde duniani, kuna mgonjwa anayesubiri kuwekewa damu ili aendelee kuishi. Aidha, kama nyote pia mnavyofahamu, hapawezi kuwa na zawadi kubwa maishani kuliko zawadi ya maisha au uhai wenyewe. Takwimu zetu zinaonyesha kuwa damu hutumika zaidi kwenye Idara ya matibabu kwa akina mama kwa 28.2%, ikifuatiwa na idara ya upasuaji kwa 23.2% na Idara ya watoto kwa 19.2%. Ni dhahiri kwamba upatikanaji wa damu ni nguzo muhimu katika kupunguza vifo vya akina mama vinavyotokana na magonjwa na uzazi na kujifungua.

Ningependa kuwatia moyo nyote mliokusanyika hapa kuwa mtu yeyote mwanaume au mwanamke anaweza kuchangia damu mradi tu awe na vigezo vifuatavyo; umri kuanzia miaka 18 hadi 65, uzito usiopunggua kilo 50 na kwa mwanamke asiwe mjamzito au anaenyonyesha. Takwimu zetu zinaonyesha kuwa 87% ya wachangia damu ni wanaume na 54% ni vijana kati ya umri wa miaka 18 hadi 29%. Tuaendelea kuwashukuru sana vijana wote wanaojitokeza kuchangi damu kwa ajili ya kuokoa maisha ya wahitaji. Chupa moja ya damu utakayochangia inaweza kugusa na kuokoa maisha ya watu hadi watatu, kwa kutengeneza mazao ya damu aina tatu: chembe nyekundu, chembe sahani na plasma.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuwekeza kwenye kuhakikisha ukuwaji wa huduma za damu salama ili zipatikane bila usumbufu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Ujenzi wa Kituo cha Kanda ya Kati Mkoani Dodoma upo katika hatua za mwisho, na inategemewa kuanza kutoa huduma mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2022/2023. Sambamba na hili Wizara ya Afya inajenga Vituo vya Mikoa, kwenye Mikoa mitano ya Kigoma, Rukwa, Njombe, Tanga na Manyara. Lengo la Serikali ya awamu ya sita ni kuhakikisha kuwa kunakuwa na Kituo cha Damu Salama ndani y a kila Mkoa. Aidha, huduma za damu salama zimeendelea kusongezwa karibu na wananchi, na kwenye kila Mkoa na Halmashauri nchini, kuna timu ya ukusanyaji damu. Serikali itaendelea kuziimarisha timu hizi na kuhakikisha hakuna mgonjwa anakosa damu.

Kupitia fedha za UVIKO-19 Wizara ya Afya itanunua magari ya kisasa ya kukusanyia damu pamoja na vifaa vya kisasa vya kukuanyia damu na mazao ya damu, na hivyo kuwezesha tiba za kibingwa na bobezi, kama upadikizaji wa viungo, kuendelea kutolewa nchini kwa tija na ufanisi.

Kipaumbele cha Wizara ya Afya ni kuhakikisha pia kuwa huduma za afya zinazotolewa zinakithi ubora unaohitajika. Mwezi wa tano, Shirika la Africa Society for Blood Transfusion kilitunuku vyeti vya ithibati kwa Kanda 6 za Mpango wa Taifa wa Damu Salama. Hii ni hatua kubwa kwa kuwa barani Afrika, ni nchi tatu tu ambazo zimefikia hatua hii, nazo ni Namibia, Rwanda na Tanzania. Cheti cha ithibati ina maanisha kuwa damu na mazao yanayopatikana kupitia vituo vya Kanda zetu inakithi viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Ndugu Wananchi, mabibi na mabwana,**

Mwelekeo wa Maadhimisho haya kwa mwaka huu 2022 unalenga kuongeza uelewa na umuhimu wa majukumu ambayo wachangiaji wa damu hutekeleza katika kuokoa Maisha na kuimarisha mshikamano ndani ya jamii zetu. Hivyo basi, Maadhimisho ya mwaka huu 2022 yana malengo yafuatayo:

- Kuwashukuru wachangia damu nchini na kujenga uelewa mpana wa jamii kuhusu umuhimu na uhitaji wa uchangiaji damu wa hiari. Maadhimisho haya yatachangia kukuza uelewa wa jamii kutambua kwamba kuchangia damu ni kitendo cha utu, huruma, upendo, umoja na mshikamano
- kuangazia umuhimu wa kujitolea uchangiaji wa damu kwa hiari ili kuwa na akiba ya damu kwa mwaka mzima na kuhakikisha wote wanaohitaji tiba ya damu katika vituo vyetu vya huduma za afya wanapata damu salama kwa wakati na muda wote kulingana na mahitaji yao
- Kutambua, kuhamasisha na kuendeleza utamaduni wa uchangiaji damu wa hiari bila malipo katika kuimarisha mshikamano na umoja wa miongoni mwa jamii;
- Kukuza uelewa wa umuhimu wa kuongeza ushiriki wa mtu mmoja mmoja, familia, vikundi, taasisi na jamii kwa ujumla ili kuongeza ukusanyaji damu kutoka

kwa wachangia damu wa hiari na hivyo kufanya huduma za damu salama kuwa thabiti na endelevu

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Maadhimisho ya mwaka huu yatatumika kufanya uzinduzi wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama kuwatumia Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kuchangia damu kwa hiari ili vituo vyetu vya huduma za afya viwe na damu ya kutosha wakati wote inapohitajika.

Wahudumu hawa watafanya kazi ya uelimishaji na uhamasishaji katika jamii kwa kupita nyumba kwa nyumba na mtaa kwa mtaa ili kusaidia kujenga utamaduni wa kujitolea damu kwa hiari miongoni mwa jamii na hivyo kufanya upatikanaji wa huduma ya damu kuwa endelevu.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Naomba nichukue nafasi hii kuwaomba wananchi wote na jamii kuendelea kujitokeza kuchangia damu kwa hiari. Viongozi wa vitongoji, viongozi wa vijiji, viongozi wa dini na taasisi mbali mbali, vikundi, akina baba na akina mama tuwe mstari wa mbele katika kuhamasisha na kuchangia damu kwa ajili ya kuokoa maisha ya wagonjwa wenye uhitaji.

Kwa kuwa tumezindua kuanza kuwatumia Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii leo niwaombe wadau wetu wa maendeleo kushirikiana na Mpango wa Taifa wa Damu salama kwa kuwafadhili ili wawezesha kufanya mafunzo kuhusu masuala ya damu salama kwa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii nchi nzima. Kwa kufanya hivi wahudumu wetu watapata uelewa na mbinu za uhamasishaji ambazo zitawasaidia kufikisha elimu sahihi kwa wanachi wengi zaidi na hivyo kuongeza kiwango cha ukusanyaji damu nchini.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Leo tunawatambua, kuwaenzi na kuwashukuru wachangia damu wote waliochangia damu na wanaendelea kuchangia damu. Damu ni uhai, na chupa moja ya damu inaweza kuokoa maisha ya hadi wagonjwa watatu, ikichakatwa ikatengenezwa mazao.

Tunawatambua wachangia damu kama wadau muhimu wa sekta ya afya. Bila ya wao kujitolea na kuchangia damu, hatuwezi kufikia malengo na kukidhi mahitaji ya nchi.

Kwa namna ya pekee nawashukuru watumishi wote wa Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama na pia Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia timu zote za damu salama za mikoa na halmashauri za wilaya kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuhakikisha uwepo wa damu ya kutosha iliyo salama na yenye viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Nawashukuru pia wadau wote: mtu mmoja mmoja, asasi za kiraia, vikundi vya kijamii, mashirika ya umma, pamoja na mashirika binafsi ambao wamewezesha ukusanyaji damu kwa namna moja au nyingine. Natambua mchango mkubwa wa waandishi wa habari ambao wamekuwa chombo muhimu sana katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuchangia damu. Vilevile, napenda kuwashukuru Serikali ya Mkoa wa Songwe, Shirika la Afya Duniani yaani WHO, Shirika la Tanzania Red Cross Society, Shirika la AMREF Afrika na wadau wengine waliochangia katika kufanikiksha mashdhimisho haya kwa mwaka huu.

**Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana**

Napenda nimalizie kwa kurudia kusema kuwa, uchangiaji wa damu ni muhimu. Huwezi kujua ni wakati gani damu unayotoa inakuwa zawadi ya uhai kwa watu wengine ambao wanahitaji kuwekewa damu haraka ili waendelee kuishi. Damu pia ina jukumu muhimu, la kuokoa maisha katika huduma ya uzazi na mtoto inapotolewa kwa wanawake walio na matatizo wakati wa ujauzito au wakati wwa kujifungua na watoto wadogo wenye hali au magonjwa yanayohitaji kuongezewa damu kwa haraka ili waendelee kuishi.

Mafanikio ya Mpango wetu wa Taifa wa Damu Salama yanawezekana tu kwa kuendeleza moyo wa kuchangia damu kwani damu haizalishwi kiwandani, bali hutolewa na wachangiaji wa damu kama ninyi mlio hapa leo. Asante kwa kujibu wito wetu wa kuokoa maisha. Tunawasihi muendelee kuwa mabalozi wetu wa damu na kuwatia moyo watu wengi zaidi kujiunga na kazi hii muhimu ya kuokoa maisha. Tukumbuke kuwa kila mtu ana haki ya kuishi na damu salama ni uhai.

## Asanteni kwa kunisikiliza!